

Bu to RAS

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

119

Anwani ya simu "TAMISEMI" DODOMA
Simu Na: (026) 2322848, 2321607
2322853, 2322420
Nukushi: (026) 2322116, 2322146
2321013,
Barua pepe: ps@pmoralg.go.tz



Tawala za Mikoa na
Serikali za Mitaa,
P.O. Box 1923,
DODOMA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. AB.194/355/01/17

07/10/2014

22/10/14

Makatibu Tawala Mikoa,
TANZANIA BARA.

**YAH: MAELEKEZO KUHUSU KUVIPATIA RUZUKU VITENGO
VYA SHERIA KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA
MITAA NA SEKRETARIETI ZA MIKOA**

Tafadhali husika na somo la hapo juu.


Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, iliitisha Kikao cha Kazi kilichofanyika tarehe 25-26/09/2014 Mjini Morogoro na kuhudhuriwa na Waziri wa Nchi TAMISEMI, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kaimu Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Naibu Katibu Mkuu - TAMISEMI, Wanasheria wa Sekretarieti za Mikoa, Wanasheria wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi zilizo chini ya OWM - TAMISEMI. Maelekezo yaliyotolewa kwenye kikao hicho, kwamba:-

- (i) Vitengo vya Sheria katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa vipatiwe ruzuku ya kuviwezesha kutekeleza majukumu yake;
- (ii) Posho ya Mavazi inayotolewa kwa Wanasheria wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mikoa na Taasisi zilizo chini ya OWM - TAMISEMI ya kiasi cha sh. 300,000/= ni kidogo, hivyo iongezwe hadi sh. 500,000/ kama ilivyo kwa Mawakili wa Serikali. OWM - TAMISEMI itawasiliana na Ofisi ya Rais Utumishi ili kupata Waraka wa ongezeko la Posho hiyo;
- (iii) Baadhi ya Halmashauri haziwawezeshi Wanasheria wake kushiriki semina, mafunzo na masomo ya kujiendeleza na hivyo kupunguza ufanisi wao wa kazi;
- (iv) Wanasheria wa Serikali za Mitaa na wale wa Sekretarieti za Mikoa kutotambuliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali chini ya Sheria Namba 4 ya mwaka 2005 inayohusu majukumu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

Kutokana na hoja hizo, mnaelekezwa kuwaelekeza Wakurugenzi kufanya yafuatayo:-

- (a) Kuhakikisha vitengo vya Sheria vinapatiwa ruzuku ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao yakiwemo ya kwenda Mahakamani, kufuatilia utekelezaji wa Mabaraza ya Ardhi na ya Kata, kushughulikia migogoro na mikataba ya Halmashauri n.k.
- (b) Kurekebisha kiwango cha posho ya Mavazi kutoka shilingi laki tatu (sh. 300,000/=) inayolipwa sasa hadi shilingi laki tano (sh. 500,000/=) kwa mwaka.
- (c) Kuhakikisha Wanasheria wanawezeshwa kuhudhuria Mahakamani, kwenye Semina na Mafunzo yanayolenga kuwajengea uwezo kama vile masomo ya Shule ya Sheria (*Law School*), mafunzo yanayohusu usimamizi wa Mikataba, Sheria ya Ubia n.k.
- (d) Wakurugenzi wawasilishe kwa Makatibu Tawala wa Mkoa maelezo binafsi ya Wanasheria (CVs) na kisha zitumwe kwa Katibu Mkuu, OWM - TAMISEMI tayari kwa kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili afanye uteuzi na kuwapa madaraka ya kuifanyia upekuzi Mikataba ya Halmashauri yenye thamani zaidi ya shilingi milioni hamsini (sh. 50,000,000) jukumu ambalo linafanywa na Mwakili wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011.
- (e) Mkoa kuanzisha CLUB za Wanasheria walioko katika Utumishi wa Umma ili Wanasheria wawe wanakutana na kujadiliana changamoto wanazokabiliana nazo. CLUBS hizo ziwe zinakutana kila robo mwaka kwa uratibu wa Katibu Tawala wa Mkoa (RAS).

Utekelezaji wa maelezo haya uanze mara moja.



Hawa A. Ghasia (Mb)
WAZIRI WA NCHI (T)

Nakala: Waziri Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu,
S.L.P. 980,
DODOMA.